# Ufundishaji wa Kiswahili Sekondari: Utekelezaji wa Muhtasari wake

*Fulgence L. Mbunda*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

## 1.0 Utangulizi

Maandalizi ya ufundishaji wa somo lolote lile huanza kwa kudurusu muhtasari wake. Muhtasari ni matokeo ya malengo ya elimu pamoja na sera za nchi kuhusu elimu katika ngazi zake mbalimbali (chekechea, msingi, sekondari, vyuo). Hali kadhalika, unatokana na malengo na sera ambazo hubainisha masomo yake mbalimbali, Kiswahili likiwamo. Mada kwa kila somo huchaguliwa na kupangiliwa kufuatana na mahitaji na matakwa ya walengwa wake. Mbinu mbalimbali za kufundishia mada teule huainishwa, na hali kadhalika, tathmini yake huonyeshwa kutokana na ufundishaji wa kila siku, mwezi, muhula na mwaka. Pamoja na hayo yote, muhtasari unaonyesha pia vifaa mbalimbali vitakavyoendana na muhtasari huo, kama vile, vitabu vya kiada, ziada na vya rejea.

Muhtasari wa Kiswahili hauwezi kukwepa wasifu uliotajwa hapo juu. Fanaka katika utekelezaji wa muhtasari wowote ule, ukiwemo wa Kiswahili, inategemea sana kuwepo kwa sifa zote zinazostahili kila muhtasari kuwa nazo. Kazi ya mwalimu katika ufundishaji itarahisishwa sana iwapo muhtasari anaopaswa kuutumia umeundwa katika misingi toshelevu na una sifa zinazostahili. Mackey (1965:323-324) anaainisha sifa nne katika muhtasari wowote ule. Kwanza, ni maudhui yake, yaani, pawepo na vipengele vyote vinavyounda muhtasari. Pili, ni uanisho, yaani, kila kipengele kinajitokeza bayana. Tatu, ni uhalali wake kufuatana na sera na malengo; na nne, ni utekelezwaji wake.

Lengo la makala haya ni kumsaidia mwalimu wa Kiswahili sekondari kumudu ufundishaji wake kwa ufanisi mkubwa akianzia na jinsi gani ataweza kuuelwa na kuutumia muhtasari wa Kiswahili kwa makini zaidi. Makala haya yanalenga hasa namna ya kumsaidia mwalimu wa Kiswahili sekondari:

(a) kuuelewa barabara muhtasari wa Kiswahili uliopo,
(b) kuoanisha ufundishaji wake na malengo ya elimu pamoja na sera za nchi kuhusu elimu,
(c) kutayarisha maazimio ya kazi kwa ufanisi zaidi baada ya kuuelewa vema muhtasari wake,
(d) kuandaa masomo yake akizingatia malengo ya elimu na sera ya elimu sekondari, na
(e) kutoa masomo yake darasani ipasavyo, kisha kutoa tathmini sahihi ya ufundishaji wake wa Kiswahili darasani.

Kutokana na mtazamo huo, makala haya yamegawanyika katika sehemu zifuatazo:

*(i)* *Muhtasari wa Kiswahili ulivyo*
Tutatumia muhtasari wa Kiswahili, kidato cha I – VI, wa mwaka 1997 kama kielezo chetu.

*(ii)* *Uchambuzi wa Muhtasari*
Tutaangalia malengo yake na mada zilizomo pamoja na muundo mzima wa muhtasari huo.

*(iii)* *Uchaguzi wa Mada*
Tutazipitia baadhi ya mada kubaini ufundishikaji wake.

*(iv)* *Mpangilio wa Mada*
Tutapitia mada kadha na kuziweka katika mfumo wa azimio la kazi.

*(v)* *Maandalio ya Somo*
Hapa tutaongelea namna mada mbalimbali zinavyoweza kuandaliwa tayari kwa kufundishwa darasani.

*(vi)* *Utoaji na Tathmini ya Somo*
Katika sehemu hii tutagusia namna ambavyo mwalimu atawashirikisha wanafunzi wake katika hali halisi ya darasani pamoja na jinsi atakavyoweza kupima ufikiaji wa madhumuni yaliyowekewa katika kipindi chochote kile.

## 2.0 Muhtasari wa Kiswahili Sekondari

Muhtasari wa Kiswahili Sekondari tutakaotumia katika mjadala huu ni ule uliotolewa na Wizara ya Elimu na Utamaduni, mwaka 1997. Muhtasari huu unachukua nafasi ya ule wa mwaka 1976 ambao ulipitiwa na kufanyiwa marekebisho yaliyoonekana yanafaa. Jambo la msingi ni kwamba muhtasari huu umetolewa baada ya kupitisha sera mpya ya elimu na mafunzo, mwaka 1995.

Utangulizi wa muhtasari huu unamshauri mwalimu kuhusu mada zilivyopangiliwa, matumizi ya mbinu anuwai za kufundishia, matumizi na utengenezaji wa zana mbalimbali za kufundishia na tabia ya kujisomea ili kutafuta mbinu mpya na kujiendeleza. Suala la mwalimu kuwa mfano limesisitizwa vilivyo katika utangulizi wa muhtasari huu.

Kimuundo, mutasari huu umeanzia na malengo ya kufundisha Kiswahili sekondari, ambayo ni haya:

(a) Kutumia Kiswahili kwa ufasaha katika fani zote za maisha
(b) Kuhakiki kazi za fasihi ya Kiswahili
(c) Kujenga tabia ya udadisi katika masuala ya lugha ya Kiswahili
(d) Kuelewa kuwa Kiswahili ni sehemu muhimu ya utamaduni wa Tanzania (uk.v).

Tumeyahariri malengo hayo kama ifuatavyo:

(1) Matumizi fasaha ya Kiswahili katika fani mbalimbali za maisha
(2) Kuzielewa kazi za fasihi na kuweza kukabiliana na maisha katika jamii
(3) Ujenzi wa tabia ya udadisi na mwelekeo chanya wa lugha ya Kiswahili
(4) Kuelewa na kupokea kuwa Kiswahili ni chombo muhimu katika kukuza na kuendeleza utamaduni wa Tanzania.

Tumesema kuwa tumeyahariri malengo hayo ili kuondoa utata na kuleta ufanisi katika ufundishaji. Mathalani, 'kuhakiki kazi za fasihi ya Kiswahili' kama ilivyo katika muhtasari siyo lengo, bali ni njia tu ya kufikia lengo katika ufundishaji wa fasihi. Kwa maana hiyo tumefikiri kuwa *kuzielewa kazi za fasihi na kuweza kuyakabili maisha katika jamii* ni lengo litakalotokana na kuhakiki kazi za fasihi.

Baada ya malengo ya jumla, muhtasari umeonyesha malengo ya kufundisha Kiswahili kwa kila kidato. Aidha, kila kidato kina mpangilio wa mada ambazo zimechaguliwa kufundishwa. Mada hizo ni kama zifuatavyo:

(i) Lugha kwa Jumla – kidato vya kwanza – sita
(ii) Fasihi – kidato vya kwanza – sita
(iii) Sarufi – kidato vya kwanza – sita
(iv) Ufahamu na Ufupisho – kidato vya kwanza – sita
(v) Utungaji – kidato vya kwanza – sita
(vi) Matumizi ya Lugha – kidato vya kwanza – sita
(vii) Historia ya Kiswahili – kidato vya kwanza – sita

Katika kila mada kuna malengo, njia na vifaa vyake vya kufundishia na kujifunzia. Kwa mfano:

| *Mada* | **Lengo** | **njia** | **vifaa** |
|---|---|---|---|
| 1. Lugha | Mwanafunzi aweze<br>♦ kutoa fasili ya lugha<br>♦ kutoa dhima ya lugha<br>♦ kutaja tanzu za lugha | Maswali na Majibu<br>Majadilia no. | Chati |
| 2. Fasihi kwa Jumla | Mwanafunzi aweze<br>♦ kutoa fasili ya fasihi<br>♦ kueleza aina za fasihi | Mifano ya kazi za fasihi na zisizo za fasihi na kuijadili | Vielezo au Vifungu vya habari vilivyo na visivyo fasihi. |

Mpangilio huu utagusiwa tena katika sehemu ifuatayo ya Uchambuzi wa Muhtasari. Jambo muhimu la kuangalia hapa ni kwamba katika safu ya Lengo kinachojitokeza wazi ni mada ndogo zitokanazo na mada kuu katika safu ya kwanza.

## 3. 0 Uchambuzi wa Muhtasari

Hii ni hatua ya kwanza kabisa katika utekelezaji wa muhtasari. Baadhi ya wataalam wamegusia muhtasari pale tu inapotakiwa kutayarisha azimio la kazi. Mathalan, katika ngazi ya uandaaji wa somo la Kiingereza, Ellis na Tomlinson (1988:316) wanashauri kuwa kabla mwalimu hajatayarisha azimio la kazi inambidi arejee kwenye muhtasari wa Kiingereza. Hii itamsaidia kupata yafuatayo: malengo ya kufundisha Kiingereza ambayo ndiyo msingi katika ufundishaji, stadi zilizomo, vipengele vya lugha vitakavyofundishwa, sehemu ambazo zinatarajiwa kuwa ngumu kwa wanafunzi, pamoja na mbinu zitakazotumiwa katika ufundishaji wake (tafsiri yangu). Hii tu haitoshi. Mbunda naye (1997:9-11) anapendekeza hatua tano za awali za kuuchambua muhtasari hata kabla ya maazimio ya kazi zikiwa ni sehemu muhimu ya misingi katika ufundishaji.

Katika uchambuzi wa muhtasari tunataka kwanza turidhishwe iwapo muhtasari una vipengele vyote. Vipengele hivyo ni pamoja na malengo ya elimu, sera ya elimu, malengo ya somo, uchaguzi wa mada, mbinu za kufundishia, vifaa vya kufundishia, tathmini ya somo, pamoja na utekelezaji wake. Utekelezaji wa muhtasari unamaanisha maandalizi ya walimu kuhusu namna ya kuutumia muhtasari huo, maandalizi ya vifaa viendanavyo na muhtasari husika, pamoja na uhusikaji wa wadau wengine, kama vile wakaguzi wa shule au wazazi. Pili, tunataka turidhike kama yaliyomo katika muhtasari yatakidhi malengo ya elimu, sera ya taifa kuhusu elimu na hali kadhalika, malengo ya ufundishaji kwa jumla, yaani, ukuzaji wa utu wote wa mwanafunzi (akili, viungo vya mwili na tabia yake).

### 3.1 Uchambuzi wa Aina ya Kwanza

Hebu tuuangalie muhtasari wetu wa Kiswahili katika uchambuzi wa aina ya kwanza, yaani, kuwepo kwa vipengele vyake vyote. Upungufu uliodhahiri katika muhtasari huu ni kwamba hauna malengo ya elimu, sera ya elimu kitaifa, sera ya elimu ya sekondari na tathmini yake. Utangulizi wake unaeleza kuwa orodha ya vitabu vya kufundishia Kiswahili itakuwa ikitolewa na Wizara ya Elimu. Vitabu vinavyotolewa na Wizara ya Elimu kila baada ya muda maalumu ni vya kufundishia fasihi andishi. Vitabu vya kufundishia Kiswahili havitolewi kila mara. Upungufu huu hauna budi kurekebishwa kwa njia yoyote ile.

Malengo ya somo yaliyopo yameelezwa bali yanahitaji kuboreshwa ili yaweze kutekelezwa kwa ufanisi zaidi kama tulivyoonesha hapo juu chini ya sehemu ya muhtasari ulivyo. Uboreshaji huo utamsaidia mwalimu kupata

uwiano mzuri katika ukuzaji wa maarifa, stadi na itikadi kama tunavyoelekezwa katika malengo ya elimu.

Uchaguzi wa mada hauna budi kuangalia haja na matakwa ya wanafunzi katika ukuzaji wa vipengele vile vitatu vya maarifa, stadi na itikadi. Mathalan, mada ya Lugha katika Kidato cha Kwanza, ina umuhimu gani kwa wanafunzi hao? Kama upo kweli, ni katika kiwango gani? Tujiulize hivyo hivyo katika mada zote zilizomo.

Lugha ina stadi nne za Kuzungumza, Kusikiliza, Kusoma na Kuandika. Stadi hizo hazijionyeshi bayana katika muhtasari. Ufupisho, kwa mfano, ni sehemu ya ufahamu, na ni matokeo ya kusoma. Ufahamu waweza kuwa wa kusikiliza au wa kusoma. Mazoezi mengine yatokanayo na kusoma hayakupewa uzito unaostahili katika muhtasari.

Mada ya Ufupisho pamoja na Ufahamu inaonekana bayana katika Vidato vya Tano na Sita tu, ingawaje ufupisho unafundishwa kuanzia Kidato cha kwanza katika mada ya Ufahamu. Mazoezi ya Ufupisho na Ufafanuzi yamekanganywa, Ufupisho unakuwa Ufafanuzi, na Ufafanuzi kuwa Ufupisho. (Tazama Kiswahili Kidato cha Kwanza, uk. 34-36). Zoezi la ufafanuzi lingeanzia na Matumizi ya Kamusi katika Kidato cha kwanza.

Muhtasari wa Kiswahili unapaswa kuwa mwongozo kwa mwalimu katika utoaji wa kila mada. Hivyo katika utangulizi wake pangeonyeshwa mbinu za jumla za ufundishaji, kama vile, mawasilisho, maigizo, majadiliano, vikundi, maonyesho na ziara; na mbinu maalum za lugha, kama vile, mbinu ya moja kwa moja ya kufundisha lugha, mbinu ya tafsiri, sarufi, vielelezo, kusoma na ya ufahamu. Katika kufanya hivyo, ile safu ya Njia za Kufundishia katika kila mada ingeboreshwa zaidi kwa kuoneshwa mbinu zote hizo.

Safu ya Vifaa vya Kufundishia imeonyesha zana za kufundishia peke yake. Muhtasari wa Misingi ya Elimu (1997) unaonyesha vifaa vya mitaala vikijumuisha muhtasari wenyewe, vitabu vya kiada, kiongozi cha mwalimu, kitabu cha mwalimu na maandiko ya rejea. Safu hii ingeonekana kama zana za kufundishia na sio vifaa. Kama ni vifaa basi tungeonyeshwa vitabu vya kiada na vya rejea kwa kila mada.

Muhtasari wa sasa hauonyeshi jinsi mwalimu atakavyoweza kukadiria maendeleo yake ya kila siku, juma, mwezi, muhula na ya mwaka. Tathmini ya Muhtasari wa Kiswahili haikujengewa ndani yake, na hivyo kumwia vigumu mwalimu kubainisha utekelezaji wake.

Suala la maandalizi kuhusu matumizi ya muhtasari uliopo na ufundishaji wa Kiswahili kwa jumla litajibiwa na kila mhusika binafsi. Wangapi, kwa mfano, wamepewa kozi maalumu kuhusu matumizi ya muhtasari huu wa mwaka 1997? Nani amepata wasaa wa kina wa kuuchambua muhtasari huu? Zipo aina ngapi za vifaa viendanavyo na muhtasari huu na kwa idadi ipi? Je, kila mwalimu wa Kiswahili anao muhtasari wa peke yake, au ni muhtasari wa kuchangia? Majibu

ya maswali haya yote yatatoa picha ya namna tulivyoandaliwa kuutumia muhtasari huo.

### 3.2 Uchambuzi wa Aina ya Pili

Aina ya pili ya uchambuzi ni ile ya kuangalia kama yaliyomo katika muhtasari wa Kiswahili yanakidhi haja na matakwa kwa walengwa. Mahitaji na matakwa hayo yamejikita katika malengo na sera zilizopo. Kwanza kabisa somo la Kiswahili halina budi kurithisha maarifa, stadi na itikadi (MSI) zilizopangiliwa na taifa katika kumkuza mwanafunzi kiakili, kimwili na kitabia.
Sera ya elimu sekondari inasisitiza malengo yafuatayo:

(1) uimarishaji na uendelezaji wa elimu ya msingi,
(2) ukuzaji wa umoja wa taifa, maadili ya taifa, heshima, utayari wa kufanya kazi, haki na,
(3) usawa wa binadamu, uraia na utamaduni wa taifa,
(4) ukuzaji wa maarifa, stadi na itikadi katika masomo mbalimbali,
(5) uwezo katika lugha na matumizi fasaha katika Kiswahili na angalau lugha moja ya kigeni,
(6) ujenzi wa moyo wa kujisomea, kujiamini na kujiendeleza,
(7) kujiandaa kwa elimu ya juu na kujiajiri. (Tazama ETP 1995, uk. 6-7)

Malengo na sera ya elimu ndizo zitakazotafsiriwa darasani katika ukuzaji wa mwanafunzi kiakili, kimwili na kitabia. Jambo la msingi ni kutambua uwiano wa malengo ya elimu (MSI) na sera ya elimu ya sekondari. Utaona kuwa ukuzaji wa umoja wa taifa, maadili ya taifa n.k. unaenda sambamba na ukuzaji wa tabia; uwezo katika lugha na matumizi fasaha katika Kiswahili yanaendana na ukuzaji wa viungo vya mwili; na ukuzaji wa maarifa unaenda pamoja na ukuzaji wa akili. Hali kadhalika, malengo ya elimu na sera ya elimu yaendane na muhtasari katika malengo ya ufundishaji, yaani, ukuzaji wa akili, mwili na tabia ya mwanafunzi. Uwiano wa malengo yote manne ya elimu, sera, somo na ufundishaji umeoneshwa hapo chini.
Uchambuzi wa muhtasari wetu utatakiwa kujibu maswali yafuatayo:

(a) Kuna uwiano gani kati ya muhtasari huu na ule wa Shule za Msingi?
(b) Somo la Kiswahili sekondari litawezaje kukuza umoja wa taifa, uzalendo, usawa, utamaduni wa taifa n.k?
(c) Kiswahili kitakuza maarifa yapi, stadi zipi na itikadi gani, na kwa namna gani?
(d) Kiswahili kitakuzwa katika viwango gani na kwa namna ipi?
(e) Kwa jinsi gani somo la Kiswahili litamwezesha mwanafunzi kujisomea, kujiamini na kujiendeleza?

(f) Somo la Kiswahili litamsaidiaje mwanafunzi kuendelea na elimu ya juu, au katika kujiajiri?

.Maana ya kuasisi sera, na hususan, sera ya elimu sekondari ni kwamba ufundishaji wa kila somo katika shule za sekondari unabidi ufuate mkondo huo. Muhtasari wa Kiswahili uliundwa katika misingi hiyo na hivyo utekelezaji wake lazima uende vivyo hivyo.

Jambo la msingi zaidi katika utekelezaji stahiki wa muhtasari wa Kiswahili ni kudhihirisha kama malengo yake yataweza kuingiliana na sera ya elimu sekondari na uwezekano wa ukuzaji wa utu wote ambao ndio mhimili pekee wa utoaji elimu popote pale. Lengo letu la kuboresha malengo ya kufundisha Kiswahili sekondari lilikuwa katika kutimiza azma hii ya ukuzaji wa akili, mwili na tabia (AMT), au urithishaji wa maarifa, stadi na itikadi (MSI). Tuone basi kwa jinsi gani haya malengo manne yaliyotolewa katika muhtasari yanavyowiana na malengo ya elimu:-

| *Malengo ya Kiswahili Sekondari* | *Malengo ya Elimu/ Kufundisha kurithisha/kukuza* |
|---|---|
| 1. Matumizi fasaha ya Kiswahili | Stadi/Mwili |
| 2. Kuelewa kazi za fasihi<br>Kukabiliana na maisha katika jamii | Maarifa/Akili<br>Itikadi/Tabia |
| 3. Tabia ya udadisi<br>Mwelekeo chanya katika lugha ya Kiswahili | Maarifa/Akili<br>Itikadi/Tabia |
| 4. Kuelewa kuwa Kiswahili ni chombo cha utamaduni wa Tanzania. Kupokea chombo hiki katika kukuza na kuendeleza utamaduni wa Tanzania | Maarifa/Akili<br>Itikadi/Tabia |

Kimsingi malengo yote manne (baada ya kuboreshwa) yanawiana moja kwa moja na malengo ya elimu. Kazi ya mwalimu itakuwa kuchagua maarifa, stadi na vipengele vya itikadi ambavyo taifa letu linataka turithishe au tukuze. Muhtasari unatuonyesha aina ya maarifa katika viwango mbalimbali, wakati sera ya taifa na ya elimu ya sekondari zinatupatia mazingira ya utoaji wa maarifa hayo. Kwa mfano, kwa kutumia vikundi na majadiliano darasani tutaweza kukuza umoja, kushirikiana, kujiamini na udadisi; vipengele ambavyo vinasisitizwa katika sera ya elimu sekondari.

Baada ya kuuchambua muhtasari vilivyo nadhani tutaweza kujibu yale maswali yaliyotolewa hapo mwanzo. Uwiano wa muhtasari huu na ule wa shule za msingi unajitokeza katika malengo sawa ya ukuzaji wa akili, mwili na tabia. Somo la Kiswahili sekondari litaweza kukuza umoja wa taifa, uzalendo, n.k. kwa kuwashirikisha wanafunzi katika vikundi na kwa kuwapa vifaa vyenye

misingi hiyo. Kiswahili kitakuza maarifa, stadi na itikadi zilizomo kwa njia ya majadiliano, maswali na majibu, vikundi, ziara, michezo, maigizo, kushirikiana na kufanya kazi kwa kujiamini na kujitegemea. Kwa kuwepo kwa vifaa vya kutosha na vya aina mbalimbali na vya viwango mbalimbali kutamwezesha mwanafunzi kujisomea, kujiamini na kujiendeleza. Katika somo la Kiswahili mwanafunzi ana nafasi ya kujiendeleza, na pia mada zake zaweza kumwandaa katika fani mbalimbali za maisha, kama vile, utunzi wa vitabu na biashara. Kwa kifupi, muhtasari tulio nao unaweza kujibu maswali yote hayo mradi tu tutakuwa makini katika kuuchambua ili tuutekeleze ipasavyo.

## 4.0 Uchaguzi wa Mada

Wataalamu mbalimbali wa ukuzaji mitaala kwa pamoja wanagusia kipengele cha uchaguzi wa mada kutokana na muhtasari kama hatua mojawapo muhimu katika ufundishaji. Mathalan, Lowman (1987:150-151) anazungumzia uchaguzi wa mada pamoja na uundaji wa malengo yake kufuatana na walengwa na mazingira yalivyo. Nao Lorger na Pierce (1983:180-187) wanasema kwamba mafanikio katika kujifunza yanategemea sana ujuzi wa mwalimu katika uchaguzi na ukutanishaji wa vipengele vya malengo, mada na shughuli husika, ambavyo vyote ni vya kufaa kwa kundi lolote la wanafunzi.

Tunakubaliana kuwa mada zilizomo katika muhtasari huu wa Kiswahili zimechaguliwa kwa makini na wataalamu mbalimbali katika kukidhi malengo ya elimu, sera ya taifa ya elimu pamoja na sera ya elimu ya sekondari. Uchaguzi wa mada unaokusudiwa hapa ni ule utakaotumiwa kufundishia darasani. Tuonavyo sisi, dhana mojawapo ya ufundishaji ni upitishaji wa maarifa, stadi na itikadi anazohitaji mwanafunzi. Msisitizo unakuwa katika mahitaji. Waamuzi thabiti wa mahitaji ya mwanafunzi ni mwanafunzi na mwalimu wake tu. Muhtasari upo pale kama mwongozo tu. Litakuwa ni jukumu la mwalimu kubaini mada zipi na katika kiwango gani zitawafaa wanafunzi wake.

Kanuni ambazo tunawashauri walimu kuzifuata katika kutekeleza hatua hii ya uchaguzi wa mada ni hizi:-

(a) Kuthibitisha umuhimu wa mada husika kulingana na mahitaji na matakwa ya wanafunzi katika kiwango kilichokusudiwa. Mathalan, mada ya 'Lugha' katika Kidato cha Kwanza ina umuhimu gani katika kiwango hiki? Inahusianaje na malengo ya kufundisha Kiswahili ya matumizi fasaha ya Kiswahili? Ni lazima kweli mwanafunzi atoe maana ya lugha, aeleze dhima ya lugha, ataje tanzu za lugha na atoe mifano ya lugha ndipo aweze kuitumia kwa ufasaha? Maswali haya na mengine mengi ndiyo ya msingi katika uchaguzi wa mada kutoka katika muhtasari. Kama kweli mada ya 'Lugha' ni muhimu kwa Kidato cha kwanza, basi ingegusia dhima/kazi ya lugha tu kutoka lugha mbalimbali wazijuazo wanafunzi hawa.

(b) Kubaini mada kuu na mada zake ndogo. Katika kanuni hii tunaichambua mada kuu katika vipengele vyake vyote.

Tuchukue mfano wa mada ya "Uundaji wa Maneno" katika Kidato cha Nne. Uundaji wa maneno ni tabia mojawapo ya lugha yoyote ile, Kiswahili kikiwemo. Mada zake ndogo zitakuwa njia mbalimbali za kuunda maneno, nazo ni:-

(i) *Kubadili mpangilio wa fonimu*

Mf: /a/e/i/k/l/m/z/ = meli, meza, mea, zama, lima, zika, zaka, kali, kuli.

(ii) *Uambishaji/Unyambulishaji wa maneno*

Mf: taifa – utaifishaji, ruka – rukia, imba – wimbo, cheza – mchezo, funga – fungana, soma – someka.

(iii) *Kuambatanisha maneno*

Mf: Mwana + hewa – Mwanahewa, Pima + maji - Pimamaji

(iv) *Kuunganisha maneno*

Mf: Mtu asiye na kwao – Msikwao, Mnyama mfu – Nyamafu, Upungufu wa kinga mwilini – Ukimwi, Mkuru wa kugenda – Mkurugenzi.

(v) *Kurudiarudia maneno*

Mf: pole – polepole, lia – lialia, cheza – chezacheza

(vi) *Kutohoa maneno ya kigeni*

Mf: mail – meli, school – skuli, jail – jela.

(vii) *Kufananisha sauti au kitu*

Mf: mzinga, chururu, ndondondo, kifaru.

Kwa mtindo huo tutaweza kukadiria idadi ya vipindi tutakavyoweza kutumia katika mada yoyote ile.

(c) Kuangalia kufundishika kwa mada. Kila mada ina maudhui ya kiasi fulani ambayo yatatosheleza katika muda fulani. Licha ya hiyo zipo mada ambazo zitahitaji zana mbalimbali. Katika kanuni hii tunatafuta vitabu vya rejea mbalimbali vyenye kuelezea mada husika, na vile vile zana mbalimbali zilizopo, na ikibidi kuangalia uwezekano wa kuzifaragua. Katika mada ya "Uundaji wa Maneno" kuna vitabu kama hivi:

- *Kiswahili Sekondari*, Taasisi ya Ukuzaji Mitaala, 1988, uk. 48 – 52.
- Sarufi ya Kiswahili, Mdee, J.S., Dar es Salaam Dar es Salaam University Press (1996), 1999 uk. 57-60.
- *Sarufi Mpya* , Mohamed, , M.A., Press and Publicity Centre, 1993, uk. 47 – 60.
- *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*, Kihore, Y.M., na wenzie, TUKI 2001, uk. 63-88, 89 – 100).

Katika mada hii mwalimu ataweza kutengeneza kadi za herufi ambazo wanafunzi watatumia kujenga maneno, mchezo wa kujenga maneno *(scrabble)* na chati mbalimbali kuonyesha uambishaji na mnyumbuliko wa maneno kama zana zake za kufundishia.

## 5.0 Mpangilio wa Mada

Umuhimu wa hatua hii umetolewa na watu kama Rowntree (1986:108) ambaye anasema kuwa lengo lake ni kuhakikisha kuwa, kila inapowezekana, mawazo wanayopambana nayo wanafunzi mwanzoni mwa somo ni yale ambayo yatawezesha, na sio kuzuia, kujifunza kwao baadaye. Na hata katika mpango wake wa ufundishaji, mwandamano wa maudhui umewekwa katika hatua ya pili, akianzia na uchaguzi wa maudhui (mada), ikifuatiwa na mbinu za ufundishaji, zana na tathmini ya somo.

Mada zilizochaguliwa katika hatua iliyopita sasa zinaratibiwa tayari kwa kuzifundisha darasani. Katika utangulizi wa muhtasari wetu (uk. iv) tunaambiwa kuwa mada zilizomo zimepangwa kulingana na vidato, lakini ufundishaji wake uwe kwa njia ya kuchanganya bila kufuata mtiririko uliomo. Ina maana kwamba katika juma moja zifundishwe mada za fasihi, utungaji na sarufi, au na ufahamu, au na matumizi ya lugha.

Hatua hii ya mpangilio wa mada inajaribu kupanga mada za ufundishaji katika muda fulani maalumu, kama ni juma, mwezi, muhula, au mwaka mzima. Kwa maneno mengine walimu wanatayarisha azimio la kazi katika muda huo maalum. Tuone sasa kielelezo cha azimio la kazi la ufundishaji wa Kiswahili katika Kidato cha Pili kwa muda wa juma moja:

| *Muda: Juma* | *Kipindi/Mada* | *Rejea* | *Mbinu* | *Maoni* |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Umbo na muundo wa vipera vya hadithi | - Kiswahili 2 uk. 1-6<br>Kiswahili Sekondari uk.119-120 | Majadiliano katika vikundi<br>Mawasilisho darasani | Muda ulitosha |
| | Maana na aina za mofimu | - Sarufi Mpya uk. 3 – 4 | Maswali na majibu | Muda haukutosha |
| | 3. Ufahamu | - Kunga za Fasihi na Lugha, uk. 59-60<br>- Kiswahili Sekondari uk. 59-63 | Kusoma kwa sauti<br>Kusikikiliza | Somo lilienda kama lilivyopang wa |

**Tanbihì**: Muhtasari hausemi unahitaji vipindi vingapi kwa juma. Vipindi vitatu vimetumiwa katika kielelezo hapo juu kufuatana na muhtasari uliopita, wa mwaka 1976.

Tunasisitiza sana suala la kutafuta rejea kwa kila mada. Taaluma kwa jumla, na hususan ya lugha, hukua na kubadilikabadilika kutokana na mapya, au utafiti. Rejea zilizotolewa katika kielelezo chetu cha azimio la kazi hapo juu ni baadhi tu ya rejea nyingi. Katika kila mada basi itatubidi kutumia rejea zote zitakazopatikana. Hii itatusaidia kupata mawazo na mifano mingi iwezekanavyo katika kumudu vipindi vyetu madarasani.

**6.0 Maandalio ya Somo**

Watetezi wa maandalio ya somo, kama vile Henson (1981), wanasema kuwa kufundisha darasa bila andalio la somo ni sawa na rubani anapoendesha ndege kwenda mahali asikokujua bila kuwa na ramani. Kwao, andalio la somo linaonyesha mwelekeo kwenye malengo ya somo. Newby na wenzie (2000) wanafananisha andalio la somo na kitabu cha mapishi, ambalo linaonesha viambato vya ufundishaji (wanafunzi, malengo, mazingira, mbinu na vifaa na zana za kufundishia) na jinsi ya kuvioanisha kufikia lengo lililokusudiwa (uk. 88). Kila anayeongelea andalio la somo hugusia vipengele vya malengo, maudhui, hatua za somo, vifaa, zana na mbinu mbalimbali za ufundishaji kwa utaratibu na uzito tofauti tofauti. Maelezo yafuatayo yanaelekeza namna ya kutumia vipengele hivyo.

Tukishatayarisha maazimio ya kazi katika muda wowote ule tutakuwa na urahisi wa kuandaa masomo yetu. Kama tujuavyo, andalio la somo lolote lile linajumuisha mada (kuu na ndogo), lengo na madhumuni yake mahsusi, rejea, zana za kufundishia na mwisho, hatua zake za kufundisha, ambazo ni utangulizi, utoaji wa maarifa mapya na hitimisho la somo. Tutatumia mfano wa mada ya 'ufahamu' kutoka azimio la kazi hapo juu kupata vidokezo vya andalio la somo.

1. Mada Kuu: Ufahamu (Kidato cha Pili)
2. Mada Ndogo: Ufahamu wa Kusikiliza
3. Lengo: Kuelewa yanayozungumzwa na kusomwa kwa sauti
4. Madhumuni mahsusi:- Kujibu maswali kwa ufasaha
   - *Kusoma kwa sauti kwa ufasaha*
5. Rejea: (a) M. Msokile – *Kunga za Fasihi na Lugha*, uk. 59 – 60.
   (a) Taasisi ya Ukuzaji Mitaala – *Kiswahili Sekondari*, uk. 59-63
   (b) Kiswahili 2, Kidato cha Pili, uk. 39-40
   (c) Mbunda/Mvungi – *Ufundishaji wa Kiswahili Sekondari*, uk. 44-48
6. Zana za Kufundishia
   (a) Kinasasauti chenye hotuba iliyoandaliwa mahsusi
   (b) Kifungu cha habari kutoka gazeti la Majira/Uhuru/Mtanzania.
7. Utoaji wa Maarifa mapya:
   (a) Utangulizi – Maswali kutokana na hotuba mbalimbali zilizosikilizwa katika nyakati tofauti

- Umuhimu wa usikivu
- Madhumuni mahsusi (Taz. Na. 4 juu)

(b) Maarifa mapya – Kusikiliza kinasasauti

- Maswali na majibu yatokanayo
- Kusoma kwa sauti (mwalimu na wanafunzi mmoja mmoja)
- Maswali kupima usikivu

(c) Hitimisho la Somo – Kujadili kanuni katika kuzungumza na kusikiliza

- Maswali ya jumla kupima usikivu.

**7.0 Utoaji na Tathmini ya Somo**

Kila mkuza mtaala, hususani katika kipengele cha ufundishaji anasisitiza tathmini ya somo kama hatua ya mwisho katika ufundishaji. Newby na wenzie (2000:220) wanatoa fasili ya tathmini kama ni mchakato wa kukusanya taarifa juu ya kufaa au ubora wa jambo fulani kama njia ya kutoa maamuzi yenye lengo la kuongeza ubora wa jambo hilo. Tathmini ni zoezi endelevu linalotumia njia mbalimbali kupima kiasi cha mwanafunzi alichojifunza pamoja na ufundishaji kwa jumla. Akina Dick na Carley (1990) wameunda mkakati wa ufundishaji unaolenga ushirikishwaji wa wanafunzi, ufuatiliaji wa shughuli za wanafunzi darasani pamoja na upimaji ili kuwezesha ufundishaji, kurekebisha ufundishaji kulingana na mahitaji ya wanafunzi pamoja na kuona maendeleo ya wanafunzi na ubora wa vifaa vya kufundishia.

Katika utekelezaji wa muhtasari wa Kiswahili itatupasa kuhakikisha iwapo mwanafunzi wa kidato chochote kile na katika mada yoyote ile anafanikisha malengo yote kwa kiasi fulani. Fanaka hii itawezekana tu kama mwalimu atajiandaa vya kutosha, yaani, atapenda wanafunzi wake wajue na watende nini na katika mazingira gani ili kukuza utu wao wote. Kwa kawaida madhumuni mahsusi yenye kumshirikisha mwanafunzi, zana mbalimbali na mazingira ya jumla darasani yatawezesha kufanikisha malengo husika.

Katika ufundishaji wa mada yoyote ile ya Kiswahili darasani kuna vihusika vikuu vitatu ambavyo vitaweza kuleta mahusiano muafaka katika kufanikisha malengo yetu, navyo ni:


(a) Mwalimu - ML
(b) Mwanafunzi, na - MF
(c) Rasilimali - RM
⟶ Mkondo wa mahusiano

Vihusika hivyo vitatu vinaweza kuathiriwa na mazingira (MZ) mengine kama vile upungufu wa vifaa, uongozi wa shule, jamii inayozunguka shule, kelele za magari na ndege, na malezi ya nyumbani.

Upo uwezekano wa kutokea mikondo mitano ya mahusiano ya vihusika hivyo katika somo lolote lile la Kiswahili, ambayo ni:-

| | | |
|---|---|---|
| (a) | ML → MF | Mwalimu anawaeleza jambo wanafunzi, anawauliza maswali, au anawaamrisha |
| (b) | MF→ ML | Wanafunzi wanamjibu mwalimu, au wanamwuliza maswali |
| (c) | MF→ MF | Wanafunzi wanabadilishana mawazo wao kwa wao, mathalan, kazi katika vikundi. |
| (d) | ML→ RM | Mwalimu anatumia zana zozote zile, kwa mfano, anaandika ubaoni, anasoma, anachora, au anaonyesha. |
| (e) | MF→ RM | Wanafunzi wanatumia zana na vifaa mbalimbali, kama vile, katika kufanya mazoezi daftarini, kusoma vitabuni, kuandika ubaoni, au kutengeneza kifaa fulani. |

Kiẹlelezo kifuatacho kinaonyesha kwa uwazi zaidi mikondo hiyo ya mahusiano:




Tunashauri kuwa kila mkondo wa mahusiano utumiwe kwa kiasi fulani katika mada yoyote ile ya Kiswahili. Mkondo ambao utatumia muda mwingi zaidi kuliko mingine utakuwa ndio unaotawala katika kipindi chochote kile. Mathalan, katika somo la 'ufahamu' tuliloandaa hapo juu shughuli muhimu itakuwa kujibu maswali ya kupima usikivu. Kwa hiyo mikondo muhimu ya mahusiano inatarajiwa kuwa MF → ML kwa kuzungumza, au MF→ RM kwa kuandika. Mikondo hiyo ndiyo itakuwa tawala (t). Mpangilio wa mikondo yote inatarajiwa kuwa hivi:-

MF → ML (t) + ML→ MF + ML → RM + MF → MF + MF → RM
Yaani, wanafunzi watatumia muda mwingi kujibu maswali ya mwalimu
MF→ RM (t) + ML→ MF→ MF→ ML + ML→ RM + MF→ MF
Yaani, wanafunzi watatumia muda mwingi kuandika (RM)

Somo la kuzungumza (majadiliano) litakuwa kama hivi:

MF→ MF (t) + ML→MF + MF→ ML + MF→ RM
Kama ni la kusimulia hadithi litakuwa:
MF→ ML (t) + MF→ RM + ML→ MF + MF→ MF + ML→ RM
Kusoma kimya na kwa sauti kutakuwa na mpangilio ufuatao:
MF→ RM (t) + MF→ ML + MF→ ML + ML→ RM + MF→ MF

Katika misururu hiyo ya mikondo, ule wenye (t) ndio unaochukua muda zaidi kufuatana na lengo la somo, na hivyo muda kupungua kwa kila mkondo unaofuata.

Kimsingi, tunarudia kusema tena kwamba kila mada ya Kiswahili ijaribu kuwa na mikondo yote ya mahusiano darasani, ndipo tutaweza kuhakikisha ufanikishaji wa malengo yetu. Katika mahusiano na vihusika mbalimbali kutakuwepo na kukuza udadisi (ML→ MF, MF→ RM, MF→ MF) kujiamini (MF→ MF, MF→ ML) kushirikiana (MF→ MF) na viungo vya mwili katika kuzungumza (MF→ ML, MF → MF), kusoma na kuandika (MF→ RM) na kufanikisha malengo ya ukuzaji wa utu wote.

Mara nyingi tathmini ya somo inaendana na utoaji wa somo. Maswali na mazoezi wakati wa somo ni kigezo tosha cha kufanikisha madhumuni ya somo husika. Kazi za kufanya baada ya vipindi nazo pia zilenge katika kufanikisha madhumuni mahususi ya somo pamoja na malengo yote kwa jumla.

Tungependa kumalizia makala haya na tathmini ambayo itagusia utekelezaji wa Muhtasari wote wa Kiswahili. Muhtasari huu tulionao, pamoja na mingine, unahitaji kuboreshwa ili uende na wakati kukidhi mahitaji na matakwa ya wanafunzi. Iwapo walimu wote wa Kiswahili tutafuata kwa makini hatua zote ambazo tumezionyesha katika makala haya, kuanzia na uchaguzi wa mada hadi utoaji na tathmini ya somo, tuna uhakika kwamba walimu watakuwa wanautathmini muhtasari wao ipasavyo na hivyo kuutekeleza sawia.

## 8.0 Hitimisho

Makala haya yamejaribu kuonyesha namna ya kutekeleza muhtasari wa somo la Kiswahili kwa sekondari. Utekelezaji huu wa muhtasari huanza na uchambuzi wa muhtasari kwa kubainisha mada mbalimbali zilizomo katika muhtasari na kuzipanga ili kuonyesha mtiririko wa ufundishaji wake, na tathmini ya somo. Kwa kuwa mlengwa katika ufundishaji wowote ule ni mwanafunzi, makala yamesisitiza kuzingatia vihusika vikuu vya ufundishaji yaani mwalimu,

mwanafunzi na rasilimali. Vihusika hivi vinapohusiana, ufundishaji huweza kufanikisha malengo ya somo yaliyowekwa.

## Marejeo


Dick, W. and L. Carely, (1990), *The Systematic Design of Instruction*, 3rd Edition. Scott, Foresman/Little, Brown Higher Education.

Ellis, R. and B. Tomlinson, (1988), *Teaching Secondary School English*, Longman.

Henson, K.T., (1981), *Secondary Teaching Methods*. D.C. Heath and Company.

Kihore, Y.M., na Wenzie, (2001) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Lorber, M.A. and W.D. Pierce, (1983) *Objectives, Methods and Evaluation for Secondary Teaching*, 2nd Edition. Prentice-Hall, Inc., Englewood Cliff, New Jersey.

Lowman, J., (1987), *Mastering the Techniques of Teaching*. New Delhi: Prentice-Hall of India.

Mackey, W.F., (1965), *Language Teaching Analysis*. Longmans.

Mbunda, F.L., (1997), 'Misingi ya Kisayansi katika Sanaa ya Ufundishaji', katika Mbunda

F.L. na T.A. Mvungi, *Ufundishaji wa Kiswahili Sekondari*, Kitivo cha Elimu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Mdee, J.S., (1996), *Sarufi ya Kiswahili*, Education Services Centre.

Mohamed, M.A., (1993), *Sarufi Mpya*. Press and Publicity Centre.

Msokile, M., (1992) *Kunga za Fasihi na Lugha*. Educational Publishers and Distributers Limited.

Newby, T.J. et al., (2000), *Instructional Technology for Teaching and Learning*, Prentice-hall, Inc.

Rowntree, D., (1986), *Educational Technology in Curriculum Development*, Paul Chapman Publishing Ltd.

Taasisi ya Elimu, (1996), Kiswahili 1–4, Oxford University Press (Mwanafunzi na Kiongozi cha Mwalimu).

Taasisi ya Ukuzaji Mitaala, (1988), *Kiswahili Sekondari*.

The Ministry of Education and Culture, (1995), *Education and Training Policy*, URT.

Wizara ya Elimu na Utamaduni, (1997) *Muhtasari wa Kiswahili, Kidato cha I – IV, V-VI*...................... Muhtasari wa Misingi ya Elimu.